East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1377

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Tamthilia ya Kiswahili katika Ukuaji na Ustawi Endelevu wa Ujasiriamali Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Tamthilia ya Safari ya Chinga (2009) ya Shani Omari

*Furaha Jumapili Masatu*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Dodoma, S. L. P. 259, Dodoma, Tanzania.
[*] Barua pepe ya mawasiliano : furahamasatu@gmail.com
**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1377**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*18 Agosti 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Ujasiriamali, Mjasiriamali, Safari ya Chinga, Dola, Tamthilia ya Kiada.*

**IKISIRI**

Ujasiriamali ni wimbo unaozidi kurindima masikioni mwa wanajamii. Wimbo huu unatokana na changamoto ya fursa funge za ajira miongoni mwa vijana. Tatizo linaonekana kuwa kubwa kwa sababu vijana wengi hawaonekani kuwa na msukumo wa ndani na wa kimazingira wa kujiajiri. Vijana wengi bado wanaamini katika kuajiriwa badala ya kujiajiri ilhali fursa za ajira rasmi wazitakazo ni chache kuliko idadi yao. Serikali na wadau wa maendeleo, wanazidi kukuna vichwa kutafuta ufumbuzi wa changamoto hii ya ajira miongoni mwa vijana. Mojawapo ya mapendekezo ya kutatua changamoto hii, ni kwa serikali na wadau kuwawezesha vijana kujikomboa kifikra kupitia elimu na mazingira rafiki kwa ujasiriamali. Baadhi ya wadau, wanaamini elimu rasmi ya ujasiriamali katika shule ya msingi na sekondari ndiyo suluhu kwa vijana kufikiria kujiajiri. Hata hivyo, kuna hoja kuwa wadau wa elimu wamechelewa sana kuiteua tamthilia ya *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari kuwa tamthilia ya kiada miongoni mwa tamthilia rasmi zinazopaswa kufundishia na kujifunza uhakiki wa fasihi na ujasiriamali katika ngazi ya sekondari na vyuo. Hivyo, makala haya yanawasilisha sehemu ya matokeo ya uchunguzi tulioufanya kuhusiana na maudhui ya tamthilia ya *Safari ya Chinga* ili kuonesha nafasi adhimu ya Tamthilia ya Kiswahili katika ukuaji na ustawi endelevu wa ujasiriamali nchini Tanzania.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1377

**APA CITATION**

Masatu, F. J. (2023). Tamthilia ya Kiswahili katika Ukuaji na Ustawi Endelevu wa Ujasiriamali Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Tamthilia ya Safari ya Chinga (2009) ya Shani Omari *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 274-288. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1377.

**CHICAGO CITATION**

Masatu, Furaha Jumapili. 2023. "Tamthilia ya Kiswahili katika Ukuaji na Ustawi Endelevu wa Ujasiriamali Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Tamthilia ya Safari ya Chinga (2009) ya Shani Omari". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 274-288. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1377.

**HARVARD CITATION**

Masatu, F. J. (2023) "Tamthilia ya Kiswahili katika Ukuaji na Ustawi Endelevu wa Ujasiriamali Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Tamthilia ya Safari ya Chinga (2009) ya Shani Omari", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 274-288. doi: 10.37284/jammk.6.1.1377.

**IEEE CITATION**

F. J., Masatu, "Tamthilia ya Kiswahili katika Ukuaji na Ustawi Endelevu wa Ujasiriamali Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Tamthilia ya Safari ya Chinga (2009) ya Shani Omari", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 274-288, Aug. 2023.

**MLA CITATION**

Masatu, Furaha Jumapili. "Tamthilia ya Kiswahili katika Ukuaji na Ustawi Endelevu wa Ujasiriamali Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Tamthilia ya Safari ya Chinga (2009) ya Shani Omari". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Aug. 2023, pp. 274-288, doi:10.37284/jammk.6.1.1377.

## UTANGULIZI

Makala haya yanaangazia nafasi ya Tamthilia ya Kiswahili katika ukuaji na ustawi wa ujasiriamali nchini Tanzania kwa kumakinikia tamthilia ya *Safari ya Chinga* (2009) ya Shani Omari. Maudhui yamegawanywa katika mada ndogo tatu kuu. Nazo ni dhana ya ujasiriamali na mjasiriamali, usuli mfupi kuhusu ulazima wa makala haya, na pia namna elimu ya ujasiriamali ilivyosanwa katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*. Lengo la makala haya ni kujibu kama tamthilia hii inafaa au haifai kuwa tamthilia teule katika kufundisha na kujifunza elimu ya ujasiriamali.

### Dhana ya Ujasiriamali na Mjasiriamali

Siyo rahisi kusema ujasiriamali na mjasiriamali ni kitu gani hasa. Hata hivyo, MoSHE (2019) wanafafanua kuwa, wanataaluma katika taaluma za biashara, maendeleo, na ujasiriamali wanakiri kuwapo kwa viashiria vya sifa na tabia zenye kutusaidia kutambua ujasiriamali na mjasiriamali ni kitu gani hasa. Kwa MoSHE, kuna mitazamo kadhaa juu ya dhana ya ujasiriamali. Miongoni mwa mitazamo hiyo ni: - (i) ujasiriamali ni mchakato wa kubainisha fursa sokoni, kuratibu raslimali zinazohitajika katika utekelezaji wa fursa husika; kisha kuwekeza raslimali ili kunufaika na fursa husika kwa maslahi mapana - ya muda mrefu. Mchakato huu unahusisha utengenezaji wa faida kupitia mapato kwa kuunganisha raslimali kwa namna mpya katika kuanzisha na kuendesha biashara. (ii) Ujasiriamali ni mchakato ambapo mtu mmojammoja anaweza kutambua umiliki wa biashara kwa kuzalisha wazo kisha kulitekeleza kutokana na ubunifu na uthubutu alioupata baada ya kung'amua fursa ambayo wengine hawaioni au wanaitumia kwa mazoea yasiyo na tija endelevu kibiashara. (iii) Ujasiriamali ni sanaa ya utambuzi wa viashiria vya kuwapo kwa fursa za biashara. Halafu kukusanya raslimali ili kuzigeuza fursa hizo kuwa biashara yenye mafanikio endelevu kupitia ubunifu, uvumbuzi, uthubutu (katika hatari ya kutofanikiwa) na mawazo / fikra endelevu.

Kwa upande wa mjasiriamali, MoSHE (2019) wanatumia mitazamo mitano (5) kumtambulisha mtu anayestahili kuitwa mjasiriamali. Kwa ufafanuzi wao, (i) mjasiriamali ni mtu yeyote anayebuni na kuendeleza wazo la biashara na kuthubutu kulitekeleza kwa kuzalisha bidhaa au huduma zenye kukidhi matakwa ya wateja pasipo kuogopa hatari ya anguko la kile anachokusudia kukitekeleza. (ii) Mjasiriamali ni mtu mweledi anayeng'amua fursa za kibiashara kwa kuzalisha bidhaa na huduma bora

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

zaidi au mpya na kubainisha namna raslimali hitajika zinavyoweza kupatikana ili kuongeza au kuleta tija kwa jamii na kwake binafsi. (iii) Mjasiriamali ni mtu mahususi mwenye uwezo wa kubaini na kutumia fursa za kibiashara; kuzikabili changamoto za kibiashara; kukuza mtaji ili kupata fedha; kuunganisha raslimali muhimu za kimiundombinu, kifedha na watu katika kukabiliana na changamoto za kibiashara; mwenye kuweka malengo kwa ajili yake na wengine; anayeanzisha vitu sahihi kwa ajili ya kujihakikishia mafanikio; na mwenye kuamini katika uthubutu pasipo kujali gharama na matokeo hasi ya uamuzi wake. (iv) Mjasiriamali ni mtu anayetengeneza ajira badala ya kutafuta kuajiriwa; mwenye maono na dira; yuko tayari kuthubutu hata kama pana hatari, na ana uwezo wa kufanya jambo litokee hata kama mazingira siyo rafiki kuwezesha utokeaji wa jambo husika.

MoSHE (2019) wanaugawa mtazamo wa tano (5) katika mitazamo midogo mitatu (3). Mitazamo hii inamakinikia uchumi, saikolojia, na falsafa ya kibepari. (i) Kwa mchumi, mjasiriamali ni yule anayeweza kuunganisha raslimali, kazi, vifaa, na aina nyingine za mali ili kuviongezea thamani zaidi vitu hivyo, tofauti na ilivyokuwa awali. Pia, mjasiriamali ni yule mwenye uwezo wa kuvumbua na kuleta mabadiliko. (ii) Kwa mwanasaikolojia, mjasiriamali ni mtu mahususi kabisa anayesukumwa na nguvu fulani ili kujipatia au kufikia jambo / kitu fulani, kuthubutu kukamilisha au kufanikisha wazo lake hata kama jambo au uamuzi wake haukubaliki miongoni mwa wabobevu na wanajamii husika. (iii) Kwa mwanafalsafa wa kibepari, mjasiriamali ni yule anayetengeneza fursa za utajiri kwa wengine, anayesaka njia bora za kutumia raslimali kwa kupunguza uharibifu na kuzalisha ajira kwa ajili ya wengine kufaidika nazo. Hapa, jamii inatakiwa kuwa kitovu cha ujasiriamali. Naye Mbhele (2012) anaongeza kuwa, ujasiriamali siyo suala la jinsi au jinsia; kwani dunia nzima inatambua wanaume na wanawake wanaweza kujishughulisha na ujasiriamali pasipo mipaka ya rika, dini, elimu, ukanda, au ukabila. Mbhele (2012) na wanataaluma wengi wa biashara na ujasiriamali wanakubaliana kuwa, wajasiriamali kote duniani ni wafanyabiashara; lakini si kila mfanyabiashara ni mjasiriamali. Kwa kifupi, ujasiriamali ni mchakato wakati mjasiriamali ni mtu anayejishughulisha na majukumu ya kiujasiriamali kama vile uanzishaji wa biashara bora kutokana na utafiti, ubunifu, na uthubutu wa kimkakati ulioendelevu daima.

**USULI**

Utalii wa kitaaluma juu ya ujasiriamali na mjasiriamali ni mwongozo kwetu katika kuchunguza na kuhitimisha kama ni kweli tamthilia ya *Safari ya Chinga* inastahili kutumika katika kufundisha na kujifunzia stadi za ujasiriamali. Tunasema hivi kwa sababu, kazi bunilizi teule na tahakiki zinazotumika kama vitabu vya kiada (lazima) ngazi ya sekondari na vyuo vya kati vinaonekana kujikita zaidi katika ukombozi wa kisiasa na kiutamaduni (Masatu, 2011). Hata hivyo, changamoto zinazoikabili dunia kwa sasa zinahitaji ufumbuzi wa kiteknolojia na kiuchumi katika kuwezesha ukombozi wa kisiasa kupata nguvu ya kuhimili minyukano ya ushindani wa kijamii na kiutamaduni (Steil na wenzake, 2002; Satpayeva na wenzake, 2022). Ripoti ya mwaka 2022 ya Shirika la Kazi Duniani (International Labour Organisation, 2022) na ile ya Umoja wa Mataifa – Divisheni ya Watu (United Nations Department of Economic and Social Affairs, Population Division, 2022) zinaonesha jinsi ambavyo nchi zinazoendelea, zinavyopitia shinikizo kubwa la umasikini wa kipato huku idadi ya watu ikiongezeka kwa kasi kinyume na kasi ya ukuaji wa uchumi na teknolojia. Na kwamba, changamoto ya ajira miongoni mwa vijana waliosoma na wasiosoma elimu rasmi inaonekana kukua kila kukicha huku fursa za ajira zikiwa haziendani na kasi ya ongezeko la wahitaji wa ajira. Ongezeko hili la idadi ya watu katikati ya lindi la umasikini, linazidi kuchochea vita ya kuhitaji fursa huru za ajira, huduma bora za jamii, usawa, demokrasia, na uwiano rafiki wa kipato kati ya walionacho na wasionacho.

Katika Tanzania, ripoti ya Juni 2020 ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaonesha hali ya ukosefu wa ajira kwa vijana wa kike mwaka 2019 ilikuwa ni asilimia 12.3

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

huku vijana wa kiume wasiokuwa na ajira ni asilimia 8.2. Wakati huohuo, ukosefu wa ajira kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 na miaka 24 ilikuwa ni asilimia 13.5 huku vijana wenye elimu ya sekondari kutokuwa na ajira ikiwa ni asilimia 13.8 juu ya wenzao wenye elimu ya msingi ambao ni asilimia 10 ya waliokosa ajira. Kwa wenye elimu ya vyuo vya kati wasio na ajira walikuwa ni asilimia 4.9 huku wenye elimu ya chuo kikuu takwimu yao haikutajwa. Tunarejelea takwimu hizi kwa sababu takwimu mpya za hali ya ajira bado hazijatolewa na Tume ya Sensa. Kwa hivyo basi, bado hatujui taifa la Tanzania lina vijana wangapi, elimu zao, hali ya ajira – kijinsia na kitaaluma. Hata hivyo, Kamisaa wa Sensa Kitaifa, Mheshimiwa Anne Makinda katika kikao kazi Jijini Arusha alinukuliwa na vyombo vya habari likiwemo gazeti la *Mwananchi* akikiri kuwa matokeo ya awali ya sensa na makazi ya mwaka 2022 yanaonesha hali ya ajira kwa vijana ni changamoto kubwa kwa sasa. Na kwamba, imefikia hatua ya kuhitaji si ukombozi wa kiuchumi, kisiasa, na kijamii pekee, bali kama taifa tunahitaji ukombozi wa kifikra, kisaikolojia na kisosholojia. Kwa sababu kuna "[…] kundi kubwa la vijana ambao hawana ajira wala hawajishughulishi na kazi yoyote ya kujiingizia kipato na ukimuuliza anasema amehitimu elimu fulani anasubiri ajira […]" (Ismail, 2022).

Baadhi ya wanataaluma miongoni mwa wadau wa maendeleo ya kisekta wakiwemo Steil na wenzake (2002); Tanzania Urbanisation Laboratory (2019), pia Satpayeva na wenzake (2022) wanaamini kuwa, umefika muda mwafaka kwa dunia na nchi mojamoja kuwekeza katika ujasiriamali wa kiuchumi na kitehama ili kuwasaidia vijana kujitambua na kujiajiri. Hivyo, ujasiriamali unapigiwa chapuo sana kama mojawapo ya njia za kupunguza nguvu ya vichocheo vya vita na umasikini duniani. Hata hivyo, wengi wanaopendekeza dunia kugeukia uwekezaji katika ujasiriamali, wanaonekana kutokutambua nafasi ya fasihi andishi katika kuchochea ukombozi wa kifikra na kimaarifa miongoni mwa wadau wa siasa, biashara, uchumi, teknolojia, na sheria. Baadhi ya wadau wa elimu na ajira nchini Tanzania, wamesikika mara kadhaa wakisisitiza elimu ya ujasiriamali ianze kufundishwa kupitia mtaala rasmi wa elimu ya shule ya msingi na shule ya sekondari. Nasi kama wanataaluma katika uga wa fasihi aghalabu fasihi andishi, hatuna budi kuchangia maarifa kwa kuwaonesha wadau mbalimbali siri ya mafanikio ya ujasiriamali iliyofumbatwa ndani ya fasihi andishi – hususani Tamthilia ya Kiswahili. Kwa hiyo, makala haya yanawasilisha sehemu ya matokeo ya uchunguzi wetu juu ya namna Tamthilia ya Kiswahili inavyotumia ubunifu endelevu kuchochea maendeleo aghalabu kupitia ujasiriamali miongoni mwa Watanzania. Ambapo, tamthilia ya *Safari ya Chinga* ikiwa rejeo mama la mjadala.

## ELIMU YA UJASIRIAMALI KATIKA TAMTHILIA YA *SAFARI YA CHINGA*

Tamthilia ya *Safari ya Chinga* imechapishwa na TUKI mnamo mwaka 2009. Tamthilia hii ina jumla ya kurasa 56. Tamthilia imejaa ucheshi. Sehemu kubwa ya lugha iliyotumika ni Kiswahili kilichofungamanishwa na lafudhi ya Kimakonde au lahaja ya Kimgao inayozungumzwa Kusini mwa Tanzania. Tamthilia hii imetungwa na mwanamama msomi wa Kitanzania anayeitwa Shani Omari (Mchepange). Yeye ni Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji. Idara hii ipo chini ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) (awali ikiitwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili - TUKI). Kwa sasa Shani Omari ndiye Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Tamthilia ya *Safari ya Chinga* inawasilisha tathmini ya mapito ya maisha ya vijana wanaopambana kujinasua kutoka lindi la ufukara kupitia ujasiriamali.

Shani Omari anatathmini kwa kina mazingira ya ukuaji na ustawi wa ujasiriamali nchini Tanzania kwa kutazama nafasi ya kila mdau muhimu katika uga huu. Wadau wakuu katika tathmini ya Shani Omari ni: - (i) dola (serikali, watunga sheria na mahakama), na (ii) mtu anayehusishwa moja kwa moja na ujasiriamali. Kiini cha makala kimegawanywa katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ya makala inajadili nafasi ya dola katika kukuza na kustawisha

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

ujasiriamali nchini Tanzania. Nayo sehemu ya pili inatazama nafasi ya mjasiriamali mwenyewe katika kukuza na kustawisha ujasiriamali nchini Tanzania. Yote haya yanatusaidia kupata picha angavu kuona iwapo maarifa na stadi zilizowasilishwa kupitia tamthilia hii zinaakisi mafunzo rasmi ya ujasiriamali ama la.

**Dola katika Kukuza na Kustawisha Ujasiriamali**

Shani Omari amefanya tathmini ya kina ili kuona namna dola inavyochochea fursa za ukuaji na ustawi wa ujasiriamali nchini Tanzania. Tathmini yake inaonesha kuwapo kwa hali na mazingira yasiyofaa miongoni mwa wajasiriamali kutokana na watendaji wengi kutokuweka mazingira na hali rafiki kwa ujasiriamali kukua na kustawi. Tathmini yake imeangazia mgawanyo wa raslimali za taifa, mazingira ya kuendeshea ujasiriamali, na mchango wa mihimili ya dola katika kukuza na kustawisha ujasiriamali. Ufuatao ni ufafanuzi juu ya mambo haya matatu.

***Mgawanyo wa Raslimali za Taifa***

Mwandishi Shani Omari anaonesha kuwapo kwa tatizo kubwa la mgawanyo usio sawa wa raslimali katika taifa kiasi cha kuathiri ukuaji na ustawi wa ujasiriamali katika maeneo yaliyonyuma kimaendeleo. Pamoja na juhudi za serikali kutoa huduma muhimu kwa wananchi, bado maeneo ya vijijini yameendelea kubaki nyuma ilhali mjini kukizidi kupiga hatua kimaendeleo (Tanzania Urbanisation Laboratory, 2019). Matokeo yake, watu wengi wanakimbilia mijini kwa kile kinachoitwa kufuata fursa za mafanikio ya maisha. Mbaya zaidi, watu waishio vijijini hawapati taarifa za kutosha na sahihi kuhusiana na maendeleo ya watu huko mijini. Hali hii inachangia kila mwenye shauku ya kufaidika na raslimali za nchi kufikiria kuhamia mjini (Tanzania Urbanisation Laboratory, 2019; Ministry of Finance and Planning, 2021). Jambo hili amelibainisha kwa kina Shani Omari kupitia kauli za Joffu na Mata. Tunanukuu: -

> ***Joffu:*** *Nasikia huko njini barabara zote zina lami. Tofauti na huku kwetu tunalima korosho lakini bado kila kitu ni shida. Maji safi, umeme, barabara nzuri bado kwetu ni kitendawili. Kazi ndo kama hivyo hakuna, kisomo hatuna. Basi maisha yamekuwa kama shubiri (uk. 8-9).[…]*
>
> ***Mata:*** *Baba, mi nkikaa hapa sidhani kama ntaendelea. Kazi sina. Umasikini unazidi kututawala. Huko njini vijana wadogo tu wanafanya biashara. Na wana maisha mazuri. Nyinyi wazee wangu mmezaliwa hapa na mmekulia hapa. Lakini mpaka leo maisha yenu ni yale yale. Hayabadiliki. Ngoja mi nende nkatafute maisha (uk. 13).*

Nukuu hizi mbili zinathibitisha kwa dhati ukubwa wa tatizo lililopo katika mgawanyo wa raslimali za taifa. Kitendo cha miji kuendelea kimaendeleo huku vijiji vikizidi kudumaa, kunaminya ukuaji na ustawi wa ujasiriamali huko vijijini. Mbaya zaidi, ujio wa watu wengi mijini kunafanya serikali ijikite katika kutatua changamoto zinazokabili sekta zote huko mjini. Matokeo yake, fedha inayokusanywa, pamoja na matumizi mengine, inabaki kukimbizana na utatuzi wa changamoto za huduma za kijamii mijini badala ya kukuza na kustawisha mazingira bora ya ujasiriamali katika kila kona ya nchi. Tanzania Urbanisation Laboratory (2019) na Ministry of Finance and Planning (2021) wanakubali kuwa kitendo cha watu wakiwemo wajasiriamali wengi kujazana eneo moja, mbali ya faida zake lukuki zikiwemo kuchochea ubunifu na mitaji, kwa upande mwingine kunaua ubunifu, mitaji na ushirikiano huku umasikini ukiongezeka maradufu. Kwa sababu kila mmoja atapambana kuhakikisha anaipata fursa nyembamba inayojitokeza hapo alipo. Na, kwa vile taifa halitakuwa limejiandaa kimkakati kupanga na kuendeleza makazi, kila mmoja ataanza kujimilikisha eneo la makazi na biashara kiholela. Mwishowe taifa litajikuta limezidiwa katika nyanja zote.

Changamoto hii husababisha kufanyika kwa uamuzi wa kikatili dhidi ya wajasiriamali na ujasiriamali kama ilivyotokea kwa wajasiriamali kuvunjiwa vibanda vyao, bidhaa kuporwa na wengine kukamatwa na kufungwa huku rushwa na dhuluma ikishamiri (uk. 50 – 51). Katika hili, Nyerere (1973)

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

anatusisitiza kuwekeza katika maendeleo ya watu badala ya maendeleo ya vitu ili kumkomboa mtu kifikra, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Nayo Independent Commission of the South on Development Issues (1992) inatuasa kuhakikisha kila eneo linazalisha na kuchochea ubunifu miongoni mwa wananchi kwa kutumia fursa na raslimali zinazowazunguka pasipo kuathiri maendeleo ya taifa na nchi. Hiki ndicho anachokiona Shani Omari kupitia tamthilia yake ya *Safari ya Chinga*.

### *Mazingira Rafiki ya Ujasiriamali*

Mojawapo ya vichocheo vya ukuaji na ustawi wa jamii katika nyanja tofautitofauti za maisha ukiwemo ujasiriamali ni kuwapo kwa mazingira rafiki ya kufanyia biashara. Ripoti ya mwaka 2022 ya Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (International Organization for Migration, 2023) inaonesha kuwapo kwa wimbi kubwa la watu wanaokimbia kutoka mazingira yasiyo rafiki kimaisha. Miongoni mwa mazingira yanayotafutwa na wahamiaji kutoka pembezoni mwa maendeleo ni mazingira salama ya kuishi, kuabudu, na kukuza mitaji. Ripoti hii inakiri hata biashara zimeathirika kwa kiwango kikubwa katika mazingira ambayo ulinzi, usalama, sera, na sheria zinazotungwa na kusimamiwa na mamlaka tofautitofauti kuanzia ngazi ya mtaa mpaka taifa hazitoi ulinzi na usalama wa mitaji, uhai na uhuru wa watu kukua na kustawi. Jambo hili linaonekana pia katika tamthilia ya *Safari ya Chinga*. Shani Omari anaonesha kuwapo kwa mazingira yasiyokuwa rafiki kwa ukuaji na ustawi endelevu wa ujasiriamali nchini Tanzania. Mwandishi anaonesha bado kodi, sera na sheria zinazotungwa siyo za kirafiki kwa wajasiriamali kukuza na kustawisha mitaji yao. Kila mjasiriamali anapojitahidi kujikuza na kujistawisha kupitia mifumo rasmi ya ufanyaji biashara, ndipo mamlaka za serikali zinapoinuka na kumfilisi kupitia kodi, sheria, wezi, vyombo vya ulinzi na usalama pia mahakama. Nukuu zifuatazo zinathibitisha haya: -

> ***Ntumusha:*** *[…]. Pia, kama una kibanda unaweza kukodisha kwa watu wengine. Biashara ya kutembeza ni nzuri na ina faida kama ukiizoea. Hulipi kodi. […]. Biashara ya kibandani pia ni nzuri. Unakuwa na mali nyingi na nsingi nkubwa ila kodi ndo inatuumiza (uk. 31).*
>
> ***Mata:*** *(Huku mate yakimtoka). Eh bwana sirikali kiboko. Kweli ikiamua jambo lake haishindwi. Yaani imesafisha jiji zima. Wamachinga, wapigadebe, machangudoa, mama ntilie, mateja, gereji bubu, vituo vidogo vya mafuta […]. (uk.50).*
>
> ***Mata:*** *[…] kitu ambacho kimeniuma ni vibaka kutuibia mali zetu. Yaani waliiba kama nyuki. Hata sijui walitoka wapi. Walinyang'anya hata kama nguo ulishika nkononi. Ama kweli kufa kufaana. Huwezi kuamini hakuna kitu tulichosevu.*
>
> ***Shukuru:*** *Si afadhali sisi tingatinga lilikuwa linabomoa?*
>
> ***Mata:****Enh?!*
>
> ***Shukuru:*** *Mama ntilie unaambiwa mugambo walibeba kila kitu. Kuanzia makreti ya soda, masufuria ya wali, mchuzi, miko, pawa, mpaka majiko ya nkaa.*
>
> *[…]*
>
> ***Mata:*** *Lazima wazimie wengine walikuwa wamekopa pesa benki. Na bado wanadaiwa madeni.*
>
> ***Hanafi:*** *Mama ntilie walitakiwa wakagomboe majungu yao kituoni. Walipofika kule walikuta majungu yameshaoshwa meupee peee! Eti yangeweza kuleta kipindupindu.*
>
> *[…]*
>
> ***Shukuru:*** *Aha! Tena siku ya operesheni safisha jiji unamwambia kabisa mansap nyumbani asipike unakuja na take away. Ndo hivyo akili kumukichwa.*
>
> ***Hanafi:*** *Vitu kama vituo vidogo vya mafuta vilivyojengwa karibu na makazi ya watu vilikuwa ni sawa kuvunjwa. Vinahatarisha usalama wa maisha ya watu na mali zao.*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

> ***Mata:*** *Lakini si hao hao wakubwa ndo walioruhusu vijengwe? Halafu baadaye wanavivunja. Huoni kama ni uonevu huo?* (uk. 51-52).

Nukuu hizi zote zinaonesha ujasiriamali ni kama tasnia haramu machoni pa mamlaka za serikali kuu na za mitaa. Kinachoonekana kusemwa na mwandishi ni kwamba, viongozi wengi hawana elimu juu ya ujasiriamali wala hawajawahi kuwa wajasiriamali. Badala ya viongozi kutengeneza mazingira rafiki ya kukuza na kustawisha ujasiriamali, wao wanawaza kukusanya kodi na mali za wajasiriamali kwa maslahi yao binafsi. Idara au taasisi za mamlaka hazionekani kuzungumza lugha moja ndani ya serikali ileile. Sheria zinaonekana kukanyagwa kwa maslahi ya muda mfupi – ama ya idara au watendaji husika. Kwa mfano, Matakala na Kwesinga (2001) wanabainisha kuwa, katika halmashauri na serikali kuu, baadhi ya maeneo hayajapangwa. Matakala na Kwesinga (2001) wanaendelea kusema, kwa maeneo yaliyopangwa, asilimia kubwa ya taarifa za mipangomiji hiyo ni mali ya walioandaa na kukabidhiwa ripoti. Ni kana kwamba, hakuna utendaji shirikishi ndani ya mamlaka au serikali. Kila mmoja anajifanyia mambo kivyake.

Ndiyo maana, watendaji wa idara ya biashara hutoa vibali vya biashara bila kujali kama eneo husika kwa kibali hicho ni rasmi au si rasmi kwa biashara. Biashara ikianza, mamlaka za huduma anuai mfano maji, umeme, kodi / ushuru na mazingira zinakuja kukusanya mapato kwa wajasiriamali bila kujali kama eneo husika ni rasmi au si rasmi kibiashara. Lakini siku moja watendaji ndani ya mamlaka za serikali, wanaibuka na kusambaratisha kwa mabavu biashara husika. Matokeo yake taifa halinufaiki, wala wananchi walio wengi hawanufaiki. Matakala na Kwesinga (2001) wanakubaliana na Shani Omari katika hili. Wanasema, viongozi wengi ni kama hawajui kipi hasa kinachohitajika kutendeka kwa faida ya jamii husika. Ni kama wanaishi katika ulimwengu tofauti na ule wanaouongoza. Ndiyo maana hata Kitambulisho cha Mjasiriamali bado hakijawa mwarobaini wa dhuluma na unyanyasaji wa wajasiriamali katika maeneo mengi ya taifa letu. Uundaji na utekelezaji wa sera na sheria ni lazima uwe chachu ya kukuza na kustawisha ujasiriamali kupitia miundombinu rafiki ya kijiografia, kibiashara, na kiufundi. Kinyume chake, hakuna ujasiriamali utakaokua wala kustawi katika mazingira ya kodi kandamizi, uporaji wa mitaji, na bomoabomoa isiyo na suluhisho mbadala linalotekelezeka kisayansi na kiuchumi.

### *Vyombo vya Kulinda Haki katika Kuatamia, Kukuza na Kustawisha Ujasiriamali*

Ukuaji na ustawi wa ujasiriamali hauwezi kuonekana katika jamii ambayo vyombo vya maamuzi na utoaji haki vinatumika kwa maslahi ya kundi dogo linalofurahia jamii ya wengi kuishi katika lindi la ufukara. Vyombo vya kulinda haki hasa bunge, mabaraza ya madiwani, polisi, mgambo na mahakama havipaswi kutunga, kuekeleza, na kutafsiri sheria ili kuwanufaisha wachache. Mahakama haina budi kutumia busara kupima misingi na mantiki ya sheria husika na athari yake kwa jamii nzima. Kitendo cha mahakama kutafsiri sheria katika ukavu wake pasipo busara kunaongeza changamoto kwa ujasiriamali badala ya kuzipunguza kama siyo kuzimaliza. Changamoto hii inawasilishwa na Shani Omari kupitia nukuu ifuatayo:

> ***Mata:*** *Mweshimiwa hakimu, sidhani kama ni kosa kufanya biashara. Nilikuwa najitafutia riziki. Na riziki ni popote.*
>
> ***Hakimu:*** *Kama riziki ni popote kwa nini usiuzie nyumbani kwako.*
>
> ***Mata:*** *Njini nilikuwa nafata wateja.*
>
> ***Hakimu:*** *Huoni kwamba ulikuwa unavunja sheria za jiji kifungu namba 005 cha mwaka 2008.*
>
> ***Mata:*** *Sikubahatika kuzisoma. Kama sheria ningepewa nikazisoma, wala nisingezivunja mweshimiwa hakimu.*
>
> ***Hakimu:*** *Kwa kuvunja sheria za usafi miji,*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

*unatakiwa kulipa faini ya shilingi laki moja. Au kifungo cha miezi mitatu jela na kazi ngumu.*

***Mata:*** *(Kwa huzuni). Mweshimiwa hakimu sina uwezo wa kulipa faini. Ndio kwanza nilianza biashara. Na sina ndugu hapa njini. Na kama ni kazi ngumu afadhali niachiwe nikapalilie mikorosho yangu Kadengwa. […].*

***Hakimu:*** *Kesi kama hii si ya kusikilizwa mara mbili. Umeshindwa leo kutoa faini unaenda ndani miezi mitatu. Ili iwe fundisho kwa vijana wengine wanaokimbilia mijini bila shughuli maalumu za kufanya.*

***Mata:*** *(Akilia na kupenga kamasi). Mweshimiwa hakimu, naomba huruma yako. Kukaa kijijini kulima pia tumechoka. Nilikuja njini kutafuta kazi. Wazazi wangu kijijini wananitegemea. Sasa kibanda changu cha biashara kimevunjwa. Mali zangu zote zimepotea. Mweshimiwa hakimu, nyie wa juu tusaidieni. Sisi vijana wenu tunataabika. Hatuna kazi* (uk. 47 - 48)

Nukuu hii inatupatia picha halisi ya namna ambavyo watoa haki wengi wanavyozitumia sheria katika ukavu wake kuhukumu pasipo kutazama matokeo ya sheria husika kwa faida ya jamii nzima na taifa. Hakimu anatoa hukumu ambayo haionekani kutatua tatizo bali kuongeza tatizo. Rekodi za International Labour Organisation (2022), International Organization for Migration (2019) zinaonesha kuwa, watu wengi hasa vijana wanazidi kuondoka vijijini na kukimbilia mijini kutafuta maisha bora. Uhamiaji huu unatokana na vichocheo vingi ikiwemo maendeleo na fursa za maisha bora kuonekana kuwanufaisha watu wa mjini kuliko wale wa vijijini. Hii ina maana kubwa kwa serikali na vyombo vya kutoa haki. Kwamba, hata hakimu akiwafunga wajasiriamali wote wasio katika maeneo rasmi, bado wataendelea kuzaliwa vijana wapya na kukimbilia ujasiriamali huko mjini.

Aidha, kutokuwekwa wazi kwa sheria na mipango miji katika nchi, pia kutokujua sheria kwa Mata na wajasiriamali wengine, hakuwapi haki ya kutokuadhibiwa. Lakini, hata kama wajasiriamali wote wangekuwa wanajua sheria husika na hiyo mipangomiji, tunaamini wasingeweza kuzitii kutokana na kutokuwapo kwa mazingira rafiki yaliyowekwa na mamlaka za miji ili kumsaidia mjasiriamali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kiufundi, hapa hakimu amethibitisha kuwa yeye binafsi ni kibaraka wa tabaka tawala badala ya kuwa mtetezi wa maslahi ya kila kundi katika jamii – hasa kundi la watu wanyonge. Dola kushindwa kutengeneza mazingira rafiki kwa watu waishio mijini na vijijini ili wajasiriamali wasirundikane mijini kiasi cha kuonekana ni uchafu kama siyo kero, kunaongeza changamoto zaidi kwa ujasiriamali kukua na kustawi haraka na kwa wepesi.

## Mjasiriamali: Mkuzaji na Mstawishaji Ujasiriamali

Ujasiriamali kama zilivyo fani nyingine maishani ina sifa, miiko na falsafa yake. Ujasiriamali ni stadi, maarifa, na tabia inayobeba ukuzaji matashi, ujasiri, kujiamini, uthubutu, ubunifu, ubahili, ushirikiano, kutokukata tamaa, kuwa na maono, utayari, busara, uadilifu kuwa mtafiti na mwenye shauku ya kujifunza daima (Drucker, 2002). Makala haya yanawasilisha kanuni chache za ujasiriamali kati ya nyingi zilizowasilishwa kitabuni.

### *Ujasiriamali ni Ubunifu, Upendo na Wepesi katika Kujifunza Mbinu za Biashara*

Shani Omari anaendelea kutoa elimu inayofungamana na falsafa ya ujasiriamali. Mjasiriamali yeyote kuanzia mchanga mpaka mkubwa lazima awe tayari kujifunza kila wakati kutoka katika nguvu ya asili na ile ya mazingirani. MoSHE (2019) wanalisisitiza jambo hili kwa uzito wa juu sana. Kwamba, kinachomfanya mjasiriamali aweze kuboresha mbinu za kupata na kuongeza kipato kupitia kazi yake ni ubunifu na kutokuona haya kujifunza kwa wengine. Aidha, mjasiriamali mjuzi na mzoefu, asione haya wala choyo kuwasaidia wengine kiubunifu na kimaarifa ili nao waweze kunyanyuka kibiashara na kimaisha. Somo hili tunalipata kupitia mazungumzo baina ya Mata na Ntumusha. Tunanukuu: -

***Mata:*** *Labda twende kwa basi. Mi nna pesa*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

*kidogo nfukoni za nkaa.*

***Ntumusha:*** *Sasa ukienda kwa basi wateja utawapataje?! Ukienda kwa basi utauza vipi? Nawe wateja wako ni watu wa majumbani?*

***Mata:*** *Ntaangalia ntakavyorudi na ntakavyoanka kesho. Kama vipi kesho ntapunzika. Ntauzia mitaa ya kule kule nyumbani.*

***Ntumusha:*** *Huwa hatufanyi hivyo. Ama sivyo biashara itakushinda. Hata hivyo utazoea tu. Ni sababu ya ugeni. Hata mi mwanzoni nlikuwa nachoka kama wewe. Nlikuwa naumwa sana mwili. Nilikuwa nameza dawa kila siku. Mwishowe nkazoea. Na wewe utazoea tu. Mwanzo ngumu.* (uk. 30)

*[…]*

***Ntumusha:*** *(Anapokea hela na kurudisha chenji). Kumbe mama hela unayo. Hutaki tu mi mwanao nipate riziki. Baba Riziki kaacha hela nyingi tu, unafanya ubahili.*

***Mteja 1:*** *Sasa unataka yote nikuachie wewe?*

***Mata:*** *Ongezea kidogo upate na viatu mama (anaonyesha viatu). Sikukuu inakuja viatu vitapanda bei. Ni bora ununue mapema*. (uk. 34-35)

*[…]*

***Ntumusha:*** *Unaona, kama nilivyokwambia unaanza bei ya juu. Halafu ndo nteja anaanza kushusha bei. Unashuka naye mpaka unapoona nawe unapata maslahi kidogo. Usianze kutaja kwa bei halali uliyonunulia. Utapata hasara.*

***Mata:*** *Sawa. Si unaona hata mimi nilivyofanya? Vile viatu bei yake ni elfu saba, lakini nimeuza kwa elfu kumi.*

***Ntumusha:*** *Pale umenifurahisha. Nilidhani ungeogopa kutaja bei ya juu. Kwa kawaida tunauza bei ya chini kama tukishapata faida ya kutosha. Kama ni jioni au siku hiyo biashara ikiwa ngumu kabisa. Bila hivyo hutaweza kupanga chumba na kujimudu kimaisha. Ndio maana tunaishi katika nyumba za bei rahisi* (uk. 36-37)

Nukuu hizi zinatupatia darasa la umuhimu wa kuwa wabunifu na wepesi wa kujifunza ili kutambua fursa na njia bora za kutatua changamoto zinazopatikana ndani ya fursa kwa sababu hakuna fursa isiyokuwa na changamoto. Ntumusha anatufundisha kuwa wavumilivu, wabunifu, wepesi wa kucheza na saikolojia ya wajasiriamali wachanga na wateja. Pia, kutokuwa na tamaa ya kupata utajiri wa haraka kupitia ujasiriamali, kutokuongozana mkiwa na bidhaa sawa, au kutokukaa eneo moja ilhali aina ya biashara na aina ya wateja inakutaka uwe mtu wa kubadilikabadilika kama kinyonga. Zaidi sana, kupitia biashara waliyofanya Mata na Ntumusha, tunafundishwa umuhimu wa kutumia lugha nzuri na yenye mvuto kwa wateja hata kama mteja hana mpango wa kununua bidhaa hiyo au kununua kwako. Aidha, kwa wajasiriamali, hata kama mnafanya biashara kwa kushirikiana, Shani Omari anatuasa kutokuwa na bidhaa za kufanana kwa 100%. Vilevile, tunafundishwa kupendana na kupeana fursa za kukua kibiashara. Kingine tunachojifunza hapa ni moyo wa mjasiriamali mzoefu kuendelea kumfundisha, kumlea na kumpongeza mwanafunzi anapofanya vizuri. Haya yote yanajengwa katika falsafa ya ubunifu, upendo na wepesi wa kujifunza kutoka kwa wengine walioona jua la ujasiriamali kabla yako. Ujasiriamali ni kushikana mikono kwa upendo, upole, uvumilivu, na utu ili wote mfanikiwe kukua na kustawi (Drucker, 2002).

### *Ujasiriamali ni Uvumilivu na Kujinyima ili Kukuza Mtaji*

Shani Omari anatufunda jambo jingine la msingi katika safari ya ukuzaji na ustawishaji ujasiriamali wetu. Shani Omari anatambua ya kwamba, kukuza mtaji siyo lelemama. Kwamba, kuna mapito yanayoweza kuathiri mtaji na safari ya ndoto yako kufa. Hivyo, mbinu nyingine ya mjasiriamali kukua na kustawi ni kujifunza namna ya kujinyima na kuvumilia. Huwezi kukuza mtaji wako endapo bomba lako la kutoa maji lina kipenyo kikubwa kuliko kipenyo cha bomba linalopokea maji hayo (Kuratko na Hodgetts, 2005). Naye Stokes (1998) anasisitiza kuwa, mjasiriamali anapaswa kuwa na tafsiri yake binafsi inayochora mstari kati ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

kujinyima / ubahili na anasa / starehe. Kamwe, mjasiriamali asiishi maisha anayoyatamani ilhali mtaji wake u duni au unaoweza kufa muda wowote. Darasa hili kutoka kwa wanataaluma hawa, halikupewa kisogo katika tamthilia ya *Safari ya Chinga* kupitia nukuu ifuatayo: -

> ***Mata:*** *Naanza kuhisi njaa. Ningepata angalau kipande cha muhogo. Mana hatujatia kitu chochote tumboni.*
>
> ***Ntumusha:*** *Mbona bado ni mapema? Ndo kwanza saa tano na nusu. Tusubiri tutembee tembee kidogo ili tule chakula cha nchana moja kwa moja. Hapa ni njini lazima ubadilishe ratiba ya kula. Wengi hatuli kutwa mara tatu. Huwa tunafanya diet. Ukikaa mwezi tu utakuwa ushazoea maisha ya Bongo.*
>
> ***Mata:*** *Unajua watu wengi wa vijijini tunafikiri maisha ya njini ni rahisi na mazuri sana.*
>
> ***Ntumusha:*** *Ni kweli lakini kwa wachache tu. Si kwa kila ntu. Walalahoi wengi maisha yetu ndo kama hivi. Beba tu hivyo hivyo utazoea. (Akimwonyesha mfuko). Huu nfuko usiutupe. Jioni tukikaribia kufika nyumbani tutawekea nguo humu. Mi ntaani kwangu wala hawajui kama ni chinga, natembeza nguo barabarani. Wananiona tu asubuhi natoka, jioni naingia kama kuku […]*. (uk. 27-28)
>
> *[…]*
>
> ***Ntumusha:*** *[…]. Nilidhani ungeogopa kutaja bei ya juu. Kwa kawaida tunauza bei ya chini kama tukishapata faida ya kutosha. Kama ni jioni au siku hiyo biashara ikiwa ngumu kabisa. Bila hivyo hutaweza kupanga chumba na kujimudu kimaisha. Ndio maana tunaishi katika nyumba za bei rahisi*. (uk. 36)
>
> *[…]*
>
> ***Mata:*** *Sawa. Lakini mi nina hamu ya wali.*
>
> ***Ntumusha:*** *Mi hupenda sana makoko ya ugali. Ukiyatia nchuzi yanalainika vizuri na unashiba vizuri.*
>
> ***Mata:*** *Sio magumu sana?*
>
> ***Ntumusha:*** *Ukizoea siyo magumu. Kila kitu ni mazoea tu. Pia, bei yake ni rahisi. Shilingi mia mbili tu, wakati sahani ya wali ni shilingi alfu.*
>
> ***Mata:*** *Ni kweli mazoea yana tabu.*
>
> ***Ntumusha:*** *Na pia anauza ndaza.*
>
> ***Mata:*** *Ndaza ndio nini?*
>
> ***Ntumusha:*** *Chakula cha jana*. (uk. 37)

Mazungumzo haya kwa namna fulani yamebeba ucheshi. Tunasema kuna ucheshi kutokana na namna Ntumusha anavyoficha ukweli wa maisha yake kwa hoja ya kupendezwa na aina ya maisha anayoyaishi. Ukitafakari "uongo" wa Ntumusha, utagundua ni sehemu ya somo la uvumilivu kama njia ya kukuza na kustawisha mtaji. Hapa Shani Omari anatufunda kuwa maadamu kujinyima huko hakuleti madhara ya kiafya, mjasiriamali hana budi kujikinai kwa kuwa bahili na mvumilivu. Si busara kula mbegu kwa njaa inayovumilika. Mjasiriamali hana budi kujikinai na kuyakinai matatizo na baadhi ya mahitaji yake na, au ya watu wanaomzunguka. Watu wengi hufa kibiashara kutokana na sababu kadhaa ikiwemo ya kushindwa kuwa wabahili na wavumilivu. Wengi wakipata fedha (hata kama ndio mtaji au mtaji na faida), badala ya kuulea mtaji, wao wanakimbilia kutatua matatizo yanayowazunguka kwa kutumia fedha ya mtaji au sehemu ya fedha ya mtaji. Matokeo yake biashara inakufa kwa kukosa nguvu ya kifedha na kiushindani (Mbhele, 2012). Kwa mujibu wa Drucker (2002), mtaji na faida yake havina budi kulindwa bila kudokolewa kwa angalau miezi sita (6) tangu umeanza kuzungushwa sokoni. Hii ina maana kwamba, hata kama kuna mahitaji yatajitokeza; kamwe mahitaji hayo yasiruhusiwe kugusa mtaji na faida yake kwa angalau miezi sita ya mwanzo. Endapo mtaji mdogo utaingia katika kutatua mahitaji nje ya biashara husika, basi jihesabu kuwa mfu kiujasiriamali (Hilrisch na Peters, 1992).

### *Ujasiriamali ni Kupanua Wigo wa Biashara kwa Kushirikiana na Wengine*

Shani Omari anatuongezea msingi mwingine wa ukuaji na ustawi wa ujasiriamali. Msingi huu ni

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

kushirikiana na wengine wenye ndoto za kupata au kukuza mitaji. Mjasiriamali hana budi kushirikiana na wengine ili kufikia malengo. Ushirikiano huu lazima uwe wenye tija kwa sababu mtu asiyekuwa na maono kama wewe au ni mbinafsi, hugeuka adui wa maono yako kiujasiriamali (Mbhele, 2012). Mbhele anasisitiza kuwa, mjasiriamali ni sharti afungamane kwa dhati na watu makini, weledi, wabunifu na wenye mafanikio katika safari ya ujasiriamali. Mazungumzo kati ya Mata na Ntumusha yanathibitisha hili. Tunanukuu: -

> ***Mata**: Ntumusha si uliniambia umefungua banda lako la mitumba?! Sasa mbona bado unatembeza nguo barabarani? Si ungeacha kutembeza?*
>
> ***Ntumusha**: Ndiyo. Lakini nimemuweka ntu ananiuzia. Ndugu yangu binamu. Pia, kama una kibanda unaweza kukodisha kwa watu wengine. Biashara ya kutembeza ni nzuri na ina faida kama ukiizoea. Hulipi kodi. Hata wewe ukiizoea utaipenda. Biashara ya kibandani pia ni nzuri. Unakuwa na mali nyingi na nsingi nkubwa ila kodi ndo inatuumiza.*
>
> ***Mata**: Itakuwaje tena uwe na kibanda na umpangishe ntu mwingine?*
>
> ***Ntumusha**: Ndo hivyo njini tunavyoishi. Maisha ni ujanja na kusaidiana. Ni kama zile nguo alizotupa Beka. Unauza na nnagawana pesa kidogo. Hivyo ni baadhi ya vitu ambavyo vinatupatia faida (uk. 31-32).*

Nukuu hii inatupatia shule bora kabisa juu ya ushirikiano. Ushirikiano mwema ni silaha ya kulinda mtaji wako. Ushirikiano mwema ni silaha ya kukuruhusu kupokea na kutoa ajira, maarifa, mitaji, mbinu, ubunifu, ujuzi, na kutanua mbawa kibiashara ambazo hukuwa nao awali. Ushirikiano mwema ni silaha ya kujenga upendo, ulinzi, uvumilivu, imani, ujasiri, na hasira ya kuishi vema duniani na akhera. Huwezi kufanikiwa katika ujasiriamali kama kila kitu utakifanya mwenyewe. Unapoanza ujasiriamali, kila jambo huwa ni geni kwako na mtaji ni mdogo. Hivyo mjasiriamali hana budi kukaa chini ya waliokwishafanikiwa ili aweze kujifunza na kukuza mtaji wake kupitia fursa wanazotengeneza waliofanikiwa (Drucker, 2002). Aidha, Drucker (2002) anasisitiza uaminifu na kutokuweka mayai katika kapu moja kwa wajasiriamali wakubwa. Vyanzo vingi vya biashara ni ulinzi wa mtaji, afya, na mali za mjasiriamali aliyekomaa kibiashara. Vyanzo vingi vyenye kusimamiwa na kuratibiwa vizuri, hukuza mtaji kwa haraka zaidi kuliko chanzo kimoja kwa sababu kila chanzo kitaleta faida katika chungu kikuu bila kusahau kuzalisha ajira kwa jamii.

Hata hivyo, Drucker (2002) anawazuia wajasiriamali wachanga kuwekeza mtaji katika fursa nyingi kwa wakati mmoja. Hii ni kwa sababu, mjasiriamali anayeanza ujasiriamali ana mtaji mdogo na hana uzoefu katika kusimamia biashara kadhaa kwa wakati mmoja au kukabiliana na changamoto za ujasiriamali. Naye Mbhele (2012) anapinga tabia ya ubinafsi na ubosi uchwara kwa sababu, baadhi ya watu wamekufa kiujasiriamali baada ya kuridhika na kile walichovuna. Hawasimamii tena biashara zao. Wamekaa na kulala nyumbani kungoja hesabu. Kila wakati mjasiriamali hana budi kuwa karibu na mitaji yake yote. Kamwe asiache ombwe la macho, masikio, akili, ubunifu, na mikono yake katika mitaji yake kuhodhiwa na watu wengine. Ujasiriamali hauumbi ubosi bali unaumba ushirikawenza (Drucker, 2002).

### *Ujasiriamali ni Kutokukata Tamaa Maishani*

Shani Omari hajasahau suala la kuishi katika kuitafuta kesho ya maono yako pasipo kuzimia roho na moyo. Kukata tamaa ni sumu kali katika safari ya kukuza na kustawisha ujasiriamali (Hilrisch na Peters, 1992; Mbhele, 2012). Aidha, wataalamu hawa wanaongeza kuwa, akili na roho yenye maono, uadilifu na juhudi ni miongoni mwa silaha za mafanikio kiujasiriamali. Shani Omari anakiri kuwapo kwa changamoto nyingi na za viwango tofautitofauti katika safari ya mafanikio ya mjasiriamali. Pamoja na kuzitambua na kuzitambulisha changamoto hizo, bado Shani Omari anatufunda na kutusisitiza kutokukata tamaa. Shani Omari anatuusia kutokuzikimbia changamoto bali tuwe tayari kuzikabili na kuzishinda. Sauti ya Shani

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Omari inasema nasi kupitia nukuu hizi: -

> ***Mata:*** *(Huku ameinamia chini). Dah! Hata sijui ntafanyaje. Nilivyokuja huku nlifikiri ntapata kazi kirahisi ili nami nipunzike kulima na kuchoma nkaa. Niwe kama wewe. Kumbe… nikishindwa kupata kazi nitafanyaje? Hela yote imeishia kwenye nauli. Kwa njomba Chupaku sikujui (Huku machozi yakimlengalenga). Ah jamani ntafanya nini?*
>
> ***Ntumusha:*** *(Akimsihi). Hapana Mata usikate tamaa… labda niende tena nikansihi anaweza akakubali* (uk. 25).
>
> *[…]*
>
> ***Ntumusha****: Ndo hivyo njini tunavyoishi. Maisha ni ujanja na kusaidiana. Ni kama zile nguo alizotupa Beka. Unauza na nnagawana pesa kidogo. Hivyo ni baadhi ya vitu ambavyo vinatupatia faida.*
>
> ***Mata****: Ikitokea siku tukagundulika na tajiri?*
>
> ***Ntumusha****: Sio rahisi. Usiwe mwoga. Wenzako wanaiba mabilioni we unaogopa hivi vijisenti tu? Bila hivyo hapa mjini hatuwezi kuishi. Ukikamatwa unalipa. (uk. 31-32)*
>
> *[…]*
>
> ***Mata:*** *Eh! Ndio nakumbuka. Ulitaka kuniambia nini vile?*
>
> ***Ntumusha:*** *Nilitaka kukwambia katika biashara kuna mambo mengi. Unaweza kuibiwa, vichochoroni vibaka wanaweza kukupora. Sasa ingetokea ukaporwa mali ungesema urudi kijijini? Hapana, tugangamale tu. Tutafanikiwa. Hata tukirudi home matatizo ni yaleyale. Mbona vijana wengi tu kama sisi wamefanikiwa? Kinachotakiwa ni uvumilivu. Mchumia juani hulia kivulini.* (uk. 54).

Nukuu hizi zinasisitiza umuhimu wa kutokukata tamaa pindi unapokutana na vikwazo katika safari ya kuatamia ndoto ya maisha yako. Pamoja na vikwazo walivyokutana navyo Sunche na Ntumusha katika kustawisha mitaji yao, bado hawaonekani kukata tamaa. Tofauti na Mata, Ntumusha ana sifa za mjasiriamali halisi. Kamwe hakati tamaa pindi anapoona fursa hata kama imejaa miiba. Mata anaonekana kupungukiwa sifa za ujasiriamali. Kila akipata msukosuko, wazo pekee linalomjia ni gundu na kurudi kijijini (uk. 54 - 56). Kwa maneno mengine, Mata hawezi kuatamia na kulea ndoto yake tunayoiona katika ukurasa wa 13 ambapo Mata anasema, "Baba, mi nkikaa hapa sidhani kama ntaendelea. Kazi sina. Umasikini unazidi kututawala. Huko njini vijana wadogo tu wanafanya biashara. Na wana maisha mazuri. Nyinyi wazee wangu mmezaliwa hapa na mmekulia hapa. Lakini mpaka leo maisha yenu ni yaleyale. Hayabadiliki. Ngoja mi nende nkatafute maisha." Matukio haya ni mazito sana kwa mjasiriamali mchanga. Pamoja na uzito wa mapito, Shani Omari kupitia Sunche na Ntumusha anatusisitiza kamwe tusikate tamaa. Pamoja na misukosuko yote inayojitokeza maishani; kama mjasiriamali, kamwe usife moyo. Shani Omari anatukumbusha kuwa maishani kuna kuteleza, lakini kuteleza huko kusigeuke mauti. Wala, kuvunjika kwa koleo kusiwe mwisho wa uhunzi kwa mjasiriamali. Daima tukumbuke ujasiriamali ni uvumilivu. Machungu na matamu yote ni sehemu ya safari ya kukuza na kustawisha ujasiliamali (Mbhele, 2012).

### *Ujasiriamali ni Ujasiri, Umakini, Kujiamini na Uthubutu*

Elimu nyingine anayoitoa Shani Omari ambayo ni sehemu ya falsafa ya ujasiriamali ni mjasiriamali kuwa mtu mwenye ujasiri, umakini, kujiamini na uthubutu. Mjasiriamali lazima ajiamini, awe makini na achukue maamuzi magumu ya kuthubutu kutekeleza kile anachokiamini. Mjasiriamali hapaswi kuogopa kutafuta, kutumia na kufaidi fursa zinazojitokeza machoni na masikioni mwake (MoSHE, 2019). Shani Omari anatufunda jambo hili pia kupitia mazungumzo kati ya Mata na Che Mundu, pia Ntumusha na Mata. Tunanukuu:

> ***Mata:*** *Baba, mi nkikaa hapa sidhani kama ntaendelea. Kazi sina. Umasikini unazidi kututawala. Huko njini vijana wadogo tu wanafanya biashara. Na wana maisha mazuri. Nyinyi wazee wangu mmezaliwa hapa na mmekulia hapa. Lakini mpaka leo maisha yenu ni*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

*yaleyale. Hayabadiliki. Ngoja mi nende nkatafute maisha.*

***Che Mundu:*** *Sawa, lakini kila ntu na bahati yake. Si kila ntu anafanikiwa maisha kiharaka hivyo. Maisha ni kutofautiana, ndio maana kuna maskini na matajiri.* (uk. 13-14)

*[…]*

***Ntumusha****: Ndo hivyo njini tunavyoishi. Maisha ni ujanja na kusaidiana. Ni kama zile nguo alizotupa Beka. Unauza na nnagawana pesa kidogo. Hivyo ni baadhi ya vitu ambavyo vinatupatia faida.*

***Mata****: Ikitokea siku tukagundulika na tajiri?*

***Ntumusha****: Sio rahisi. Usiwe mwoga. Wenzako wanaiba mabilioni we unaogopa hivi vijisenti tu? Bila hivyo hapa mjini hatuwezi kuishi. Ukikamatwa unalipa (uk. 31-32)*

Nukuu hizi zinaonesha umuhimu wa mjasiriamali kusimamia kile anachokiamini hata kama kuna mawazo mbadala yenye kukatisha tamaa au kuibua mazingira ya kuogofya. Mjasiriamali ni lazima awe tayari kuzikabili changamoto na kuatamia maono yake hata kama mbele yake hakuonekani nuru. Wizi siyo jambo jema maishani. Hata hivyo, katika kukuza mtaji, mjasiriamali hana budi kutafuta bidhaa za bei nafuu zaidi kwa njia rasmi na zisizorasmi huku akichukua tahadhari za kutokupoteza uaminifu. Kidini, wizi haukubaliki (Kutoka, 20:15 katika Bible Society of Tanzania, 1997), lakini katika mazingira yanayoruhusu upatikanaji wa bidhaa kwa bei nafuu mjasiriamali hana budi kuchangamkia fursa kwa ujasiri, umakini, kujiamini na kuthubutu. Ubunifu na ujasiri katika kupata huduma na bidhaa kwa bei nafuu zaidi kisha kuuza kwa bei ya juu husaidia kukuza mtaji kwa haraka (Drucker, 2002).

### *Ujasiriamali ni Kutathmini Mambo ili Kuepuka Hatari na Hasara Zinazoepukika*

Shani Omari anatuasa kuepuka mambo yanayoweza kusababisha kudumaa au kufa kwa maono ya, na ujasiriamali wenyewe. Miongoni mwa mambo hayo ni kiburi, dharau na ujuaji. Mjasiriamali ni sharti uwe mtulivu na mwenye busara ili kuongoza tathmini ya kisayansi. Si kila wakati unahitaji kutumia nguvu na uthubutu usiohesabu gharama. Maguvu, ujuaji na jeuri havijawahi kuleta matokeo chanya katika mambo yenye mkono wa mtu mwenye nguvu zaidi yako (Mbhele, 2012). Hata kama unaonewa, busara na utulivu ni sharti vikuongoze katika kufikia ufumbuzi wa changamoto husika ili uweze kukuza na kustawisha ujasiriamali wako. Shani Omari anaonya juu ya mabavu yasiyoongozwa na utulivu wala busara; kupitia kauli za Ntumusha mbele ya Mugambo 1, na mazungumzo baina ya Mata na Shukuru. Tunanukuu: -

***Mugambo 1:*** *(Akimfuata Mata na kumpiga virungu usoni). We ndo unajifanya jeuri eh.*

*[…]*

***Vijana:*** *[…]. (Vumbi limetanda. Sauti ya tingatinga inasikika ikiendelea kuvunja vibanda. Sasa linavunja kibanda cha Ntumusha).*

***Ntumusha:*** *(Amesimama pembeni na baadhi ya vitu vyake. Amechanganyikiwa. Anaifuata sauti ya tingatinga inapotokea. Niueni niueni! Nasema niueni. […] (Sauti ya tingatinga inazidi. Ntumusha bado amesimama. Sauti inazidi kuongezeka. Ntumusha anakimbia kwa hofu na woga. Anaanguka na kuangusha baadhi ya vitu alivyoshika. Anainuka na kukimbia huku akichechemea. Anatoka).*

***Vijana:*** *(Wamejaa vumbi. Wanaokota mali za Ntumusha bila kuogopa tingatinga wala Mugambo). […]* (uk. 45 - 46).

***Mata:*** *[…] kitu ambacho kimeniuma ni vibaka kutuibia mali zetu. Yaani waliiba kama nyuki. Hata sijui walitoka wapi. Walinyang'anya hata kama nguo ulishika nkononi. Ama kweli kufa kufaana. Huwezi kuamini hakuna kitu tulichosevu.*

*[…]*

***Shukuru:*** *Mama ntilie unaambiwa mugambo walibeba kila kitu. Kuanzia makreti ya soda, masufuria ya wali, mchuzi, miko, pawa, mpaka*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

*majiko ya nkaa*. (uk. 51)

Nukuu hizi zinaonesha hasara waliyoipata wajasiriamali baada ya kushindwa kutii tangazo la amri ya kuondoka katika mazingira yasiyorasmi kwa shughuli za ujasiriamali. Ni kweli kwamba, kosa ni la serikali kushindwa kuandaa mazingira rafiki kwa wajasiriamali kufanya kazi zao bila bughudha kutoka kwa mamlaka na wateja. Hata hivyo, kama wajasiriamali, bado walikuwa na nafasi ya kuishi kama paka na panya. Kupitia tamthilia hii, Shani Omari anatujuza kuwa wajasiriamali wote walipewa taarifa kupitia redio na gari la matangazo. Kila mmoja alitakiwa kuondoka katika maeneo yasiyorasmi kisheria na kuelekea kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za ujasiriamali. Taarifa hiyo ilitolewa na kurudiwa mara kadhaa - siku kadhaa kabla ya oparesheni safisha jiji. Hata siku mahususi ya kusafisha jiji ilitamkwa kupitia redio (uk. 42). Katika hili, Ntumusha, Mata, na wajasiriamali wengine hawakutumia akili na busara bali maguvu yasiyo na tija. Mjasiriamali anapaswa kujitetea kwa kila hali lakini busara lazima iongoze tathmini ya mapambano kuepuka hasara ya kiwango cha juu na cha kutisha. Mjasiriamali halisi hawezi kutumia maguvu bila akili kamwe (Mbhele, 2012).

## HITIMISHO

Makala haya yamewasilisha kwa kirefu namna Shani Omari alivyotumia kalamu na karatasi ya kifasihi kuchangia katika kutoa tathmini ya mazingira na elimu ya ujasiriamali kwa wasomaji wake. Tamthilia ya *Safari ya Chinga* ikitazamwa kwa jicho la kitaaluma, kisera, na kisheria itakuwa ni chanzo kimojawapo muhimu katika kumkomboa, kumkuza, na kumstawisha mjasiriamali wa Tanzania. Tunapendekeza kwa mamlaka za elimu nchini Tanzania zinazojihusisha na elimu, fasihi na ujasiriamali kukiteua kitabu hiki kuwa moja ya vitabu vya lazima vya kusomwa na kutahiniwa katika mitihani ya kidato cha nne, kidato cha sita, vyuo vya kati na vyuo vikuu katika madarasa ya kozi za fasihi na kozi za ujasiriamali. Hata katika warsha, semina na makongamano ya ujasiriamali, kitabu hiki hakina budi kurejelewa na ikiwezekana kuwahamasisha washiriki kukinunua na kukisoma kwa jicho la ujasiriamali. Tathmini ya Shani Omari kupitia tamthilia yake ya *Safari ya Chinga* ikipokelewa kwa mikono miwili na kutekelezwa kwa usahihi miongoni mwa wajasiriamali na mamlaka za nchi katika ngazi zote, ujasiriamali utakua na kustawi badala ya kudumaa na kusuasua.

## MAREJELEO

Bible Society of Tanzania. (1997). *Maandiko matakatifu ya Mungu yaitwayo BIBLIA.* Nairobi: Africa Area Typesetting Unit.

Drucker, P. F. (2002). *Innovation and entrepreneurship: Practice and discipline* (Adobe Acrobat E-Book Reader edition v 1). Toronto, Canada; London, UK: HarperCollins Publishers Ltd.

Hilrisch, R. D., & Peters, M. P. (1992). *Entrepreneurship: Starting, developing and managing a new enterprise* (2nd Edition). Boston: Irwin Homewood.

Independent Commission of the South on Development Issues. (1992). *The challenge to the south: The report of the South Commission.* Oxford University Press.

International Labour Organisation. (2022). *World employment and social outlook: Trends 2022*. Geneva: International Labour Office.

International Organization for Migration. (2023). *World migration report 2022*. https://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2023.pdf.

Ismail, B. (Jumatano, Oktoba 12, 2022). Makinda awataka vijana kujitafutia ajira wenyewe. Katika *Mwananchi*.

Kuratko, D. F. & Hodgetts, R. M. (2005). *Entrepreneurship: Theory, process, practice* (6th Edition). Thomson South – West.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Masatu, F. J. (2011). Ufundishaji wa Nadharia za Uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili katika Tanzania. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma. Haijachapishwa.

Matakala, P. & Kwesinga, F. (2001). Community needs and demands and their actual involvement in forest management. Katika Stisen Müller, B., S. na wenzake (Wah.), *Proceedings from the Danida DANCED workshop on sustainable forest management in Southern Africa*, Windhoek, Namibia.

Mbhele, T. P. (2012). The study of venture capital finance and investment behaviour in small and medium-sized enterprises. *SAJEMS NS* 15 (1). 94 – 111.

Ministry of Finance and Planning. (2021). National five-year development plan 2021/22-2025/26: Realising competitiveness and industrialisation for human development. ___

MoSHE. (2019). *Entrepreneurship*. Addis Ababa: _____

Nyerere, J. K. (1973). *Uhuru na maendeleo*. Oxford: Oxford University Press.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu. (2020). 2019 Tanzania kitarakimu. https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/refrences/Tanzania_in_Figures_2019.pdf.

Omari, S. (2009). *Safari ya Chinga*. Dar es salaam: TUKI.

Satpayeva, Z., Kangalakova, D., Ibraimova, S., & Utemissova, G. (2022). The Science Impact on Country's Socio-Economic Development. *Eurasian Journal of Economic and Business Studies*, *3*(65), 27-46. https://doi.org/10.47703/ejebs.v3i65.142.

Steil, B., Victor, D. G., & Nelson, R. R. (2002). *Technological innovation and economic perfomance*. Oxford: Princeton University Press.

Stokes, D. (1998). *Small business management* (3rd Edition). London: Continuum.

Tanzania Urbanisation Laboratory. (2019). *Harnessing urbanisation for development: roadmap for tanzania's urban development policy. paper for the coalition for urban transitions.* London and Washington DC. http://newclimateeconomy.net/content/cities-working-papers.

United Nations Department of Economic and Social Affairs, Population Division. (2022). *World population prospects 2022: Summary of results*. UN DESA/POP/2022/TR/NO. 3.